**6 JUNI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### Kikao cha Arobaini na Moja – Tarehe 6 Juni, 2025

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, sasa aulize swali lake, kwa niaba yake.

Na. 521

### Ujenzi Shule za Sekondari Bulamba na Nansimo – Mwibara

**MHE. KASALALI E. MAGENI K.n.y. MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Shule za Sekondari Bulamba na Nansimo ili zitoe elimu ya kidato cha tano na sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Sekondari Nansimo ilipata kibali cha kupokea wanafunzi wa kidato cha tano kwa barua yenye Kumb. Na. EB.280/315/3816/10 ya tarehe 20/11/2023 ambapo jumla ya wanafunzi 176 wa kidato cha tano walipangiwa mwezi Julai, 2024. Aidha, shule tatu za Halmashauri ya Wilaya ya Bunda zikijumuisha Chitengule ya Jimbo la Mwibara zipo kwenye mpango wa kupandishwa hadhi kuwa na kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025 Serikali imetoa shilingi milioni 130 kwa ajili ya ujenzi wa bweni moja katika Shule ya Sekondari Chitengule kwa ajili ya maandalizi ya kuipandisha hadhi kuwa ya kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika shule za sekondari zilizo kwenye mpango wa halmashauri kwa ajili ya kupandishwa hadhi kuwa za kidato cha tano na sita.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kasalali.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri kwa niaba ya watu wa Mwibara, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Shilanona katika Jimbo la Sumve kimeanza ujenzi wa shule ya sekondari ambayo mpaka sasa Mfuko wa Jimbo na wananchi tumeshatumia zaidi ya shiingi milioni 70 na shule ile bado haijaisha.

Je, ni lini Serikali itatupatia pesa kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa shule ile ili watoto wa Shilanona ambao wanatembea umbali

mrefu kwenda Shule ya Sekondari Wala, waweze kupata huduma ya sekondari karibu?

Swali la pili, Shule ya Sekondari ya Wala ni shule ambayo ina wanafunzi wengi sana, na imefika hadhi ya kuwa na kidato cha tano na sita. Je, ni lini Serikali itaongeza majengo na kuipandisha hadhi shule hiyo iwe ya kidato cha tano na cha sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza ninawapongeza sana wananchi wa Jimbo la Sumve pamoja na Mheshimiwa Mbunge Kasalali Mageni, kwanza kwa wananchi kuchangisha michango yao kwa ajili ya kuanza ujenzi wa shule hii ya sekondari kwa kidato cha kwanza hadi cha nne, lakini pia Mheshimiwa Mbunge kupeleka fedha pale za Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, kwa sababu umeshawasilisha hoja hiyo Serikalini na Serikali hii sikivu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumeshachukua hoja ya wananchi wa Sumve, tumeshaiweka kwenye Mpango wa *SEQUIP* kwa ajili ya kupeleka fedha ili tuweze kuikamilisha Shule hiyo ya Sekondari ya Shilanona. Kwa hiyo, ninaomba tu nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Sumve kwamba Serikali inalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, zipo shule nyingi ambazo zina sifa ya kuwa kidato cha tano na cha sita ikiwemo shule ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja kwa idadi ya wananchi pia kwa uhitaji wenyewe wa shule ya kidato cha tano na sita, nikuhakikishie tu kwamba, kupitia mpango wa *SEQUIP* tumeainisha maeneo yote ya kipaumbele kwa ajili ya kuanza kujenga shule za kidato cha tano na sita na tutatoa kipaumbele katika shule hiyo ili iweze kujengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika Jimbo la Tarime Vijijini unakuta kuna shule moja ina walimu watatu wa Kiswahili, lakini shule jirani haina Mwalimu wa Kiswahili, halafu shule nyingine ina walimu wawili wa hesabu, lakini shule nyingine haina mwalimu wa hesabu, hivyo hivyo katika masomo mengine.

Je, Serikali ipo tayari kutoa mwongozo na maelekezo mahsusi pale Tarime Vijijini ili wafanye msawazo, palipo na upungufu wa walimu kwa masomo fulani walimu wapelekwe ili wanafunzi wote kwa pamoja waweze kupata elimu inayofanana na wafanye mitihani sawasawa, ili waweze kufanya vizuri katika mitihani yao? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali ilishatoa mwongozo, kwanza kuhakikisha kwamba shule katika halmashauri na mikoa yetu zinakuwa na usawa katika upatikanaji wa walimu wa masomo mbalimbali wakiwemo walimu wa masomo ya hisabati na masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kwa sababu ni wajibu wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tarime, ni wajibu wa Afisa Elimu Sekondari na Msingi wa Halmashauri ya Tarime, pia ni wajibu wa *REO* - Afisa Elimu wa Mkoa wa Mara. Nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tarime kwamba ndani ya wiki mbili wapitie shule hizo ambazo zina walimu wengi zaidi wa hisabati na sayansi na waangalie zile shule ambazo zina walimu wachache zaidi ili wafanye msawazo wa ndani wa kuhamisha walimu kwenda kwenye shule ambazo hazina walimu kabisa, wakati Serikali ikiendelea kuandaa vibali kwa ajili ya kwenda kuziba *gap* la watumishi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, Kata ya Nzihi katika Jimbo la Kalenga ina shule za sekondari mbili, lakini watoto wanakwenda mbali sana kutafuta masomo ya kidato cha tano na cha sita; je, ni mpango gani wa Serikali kutupatia shule ya kidato cha tano na cha sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vipaumbele vya Serikali ni kuhakikisha tunasogeza huduma za elimu karibu zaidi na jamii na wanafunzi ili kuepuka wanafunzi kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za kidato cha tano na sita.

Kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Kiswaga kwamba Serikali kupitia mpango wa *SEQUIP* imeendelea kuainisha maeneo yenye uhitaji wa shule za kidato cha tano na sita, tutaipitia pia Kata ya Nzihi katika Jimbo la Kalenga ili kuona katika eneo hilo ni eneo gani linafaa kuwa na kidato cha tano na sita, moja ya shule hizo tunaweza kupandisha hadhi ikawa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, waanze kufanya tathmini hiyo kupitia wataalam wake na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI, lakini pia kuanza kutenga mapato ya ndani kwa awamu kwa ajili ya kuanza kujenga baadhi ya miundombinu wakati Serikali pia ikitafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ikupa Alex.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba kuna utoshelevu wa walimu wa elimu maalum? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha miundombinu ya elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, pia walimu ambao wanafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum na ndiyo maana vipo vyuo ambavyo vinafundisha walimu wenye uwezo wa kwenda kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum, lakini zipo shule ambazo zina miundombinu maalum kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Stella Ikupa kwamba kama ambavyo Serikali imeendelea kuboresha miundombinu, walimu pamoja na vifaa vya kujifunzia na kufundishia wanafunzi wenye mahitaji maalum, itaendelea kufanya hivyo na kila kwenye bajeti ya kila mwaka wa fedha ikiwemo bajeti ya mwaka ujao 2025/2026, bajeti hiyo imetengwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaboresha mazingira ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera, sasa aulize swali lake.

Na. 522

**Muswada wa Sheria Kuhusu Changamoto za Muungano zilizopatiwa Ufumbuzi**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali italeta muswada wa sheria kuhusu changamoto za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi ili sasa ziwe kwa mujibu wa sheria?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa mpaka sasa jumla ya changamoto 22 za Muungano zimekwishapatiwa ufumbuzi. Aidha, katika Kikao cha Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ambacho kilifanyika tarehe 4 Aprili, 2025 Ikulu Dar es Salaam kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi wa changamoto za Muungano, kilitoa maelekezo kwa Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kulifanyia kazi jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mara baada ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa taarifa hiyo, itatolewa kwa umma, ninakushukru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zahor.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, kwanza ninaomba niishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri, lakini ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa sababu bado Tanzania ipo na itaendelea kuwepo, Muungano upo na utaendelea kuwepo. Je, ni vipi hasa vigezo vinavyotumiwa na Serikali kuweza ku-*identify* kwamba hii ni changamoto ya Muungano, kwa sababu kila siku zinakuja mpya?

Swali la pili, je, Serikali sasa iko tayari *seriously* kuanza kutoa elimu kwa wananchi wa Tanzania ili waweze kuelewa changamoto zote ambazo zimepatiwa ufumbuzi? Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali

mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Jimbo la Mwera, lakini kabla ya hapo nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana kwa kuwa amekuwa mdau mzuri na ni mmoja wa miongoni mwa watu ambao wanaendeleza, kuutunza na kuuenzi Muungano huu kwa vitendo kwa kutaka kujua mambo mbalimbali ya Muungano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme tu kwamba, kabla ya yote ninataka nichukue fursa hii niwambie Watanzania kwamba si kila changamoto ni changamoto ya Muungano. Zipo changamoto ambazo tunasema hizi tuzipeleke tukazijadili, lakini zipo nyingine ni changamoto za sekta zenyewe kukaa zikalimaliza ili zisiwe changamoto ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vigezo ambavyo huwa tunavichukua; cha kwanza ni kigezo cha kisekta, endapo kumetokea changamoto na sekta zimekaa lakini zimeshindwa kufikia muafaka, hapo zinakuja kwetu kama Ofisi ya Makamu wa Rais tunaosimamia Muungano, halafu sisi tunazijadili, tunazipeleka ngazi ya watalaam, ngazi ya Makatibu Wakuu, Mawaziri halafu zinakwenda kwenye ngazi ya kutatuliwa, kwa hiyo, hicho ni kigezo kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kigezo cha pili ni kigezo cha hali ya wakati ule. Kuna hali fulani zinajitokeza hizo zinakuwa ni kigezo kwamba hatuna namna ya kufanya, lazima tuzifanye sasa iwe ni sehemu ya kusema hiki ni kigezo cha kupelekwa kwenye hoja za kujadiliwa kama hoja za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni uzito wa hoja yenyewe, na ndiyo pale niliposema kwamba siyo kila hoja au changamoto itakuwa ni changamoto ya Muungano. Ziko hoja nzito ambazo tunasema hizi tuzijadili, zipo zingine tunasema hizi tuzimalize katika namna ambayo hazitoingia katika orodha ya changamoto za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali iko tayari na kazi hii imeshaanza. Tumefanya kazi kubwa katika kuielimisha jamii juu

ya suala zima la Muungano huu, faida, fursa, asili na chimbuko la Muungano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya habati vimetusaidia sana, magazeti, televisheni, *radio*, mitandao ya kijamii, na makongamano mbalimbali. Tumetoa vitabu vya Muungano, mijadala mbalimbali, majarida na ziara za mafunzo zinazowafanya watu wajifunze kuhusu Muungano, ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika ni lazima tujivunie Muungano tulionao kati ya Zanzibar na Tanganyika na kuweza kuifanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka 60 sasa tangu tumekuwa na Muungano huu, hivi sasa Serikali haioni kwamba, inao uzoefu wa kutosha pale inapobaini changamoto na kujipa muda mchache sana wa kuweza kuzitatua badala ya kukaa kipindi kirefu mpaka hoja inakuwa ni changamoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Abbas, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru na kumpongeza kwa kazi kubwa anayoifanya hasa kwenye haya mambo ya Muungano. Ninataka niwaambie Mheshimiwa Mbunge, Wabunge na Watanzania wote kwamba Muungano huu ni wa nchi mbili, Muungano huu ni wa Tanganyika na Zanzibar. Muungano unapoitwa Muungano maana yake siyo hoja iibuke tu tuijadili kwa muda mfupi tuimalize, kinyume na hapo tunaweza tukatengeneza changamoto ndani ya changamoto, ndiyo maana tunakwenda hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatoka hatua za kisekta, tunakuja hatua za Makatibu Wakuu, tunapita kwa wataalam, tunakuja hatua za Mawaziri na tunakuja sasa hatua kubwa ambayo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri, lengo na madhumuni ni kwamba tunapotatua changamoto iwe tumeitatua na tusonge mbele ili tufanye mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuchukua ushauri wake ili zile zinazochukua muda hazitachukua muda na zile ambazo tunahisi zitachukua muda mrefu tutakwenda nazo kwa mujibu wa taratibu, lakini zile ambazo tunahisi ni za kufanya tu haraka tufanya, ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata ambalo ni swali la Wizara ya Maji. Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 523

**Mradi wa Maji Kata ya Kalulu**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha mradi wa maji katika Kata ya Kalulu ili kumtua mama ndoo kichwani na kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 itaanza utekelezaji wa mradi wa maji wa Kata ya Kalulu uliopo Wilayani Tunduru, Mkoa wa Ruvuma. Kazi zinazotarajiwa kutekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa nyumba mbili za mitambo *(pump house),* ufungaji wa pampu za kusukuma maji, ujenzi wa matanki mawili yenye ujazo wa lita 50,000 kila

moja, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 13, sanjari na ujenzi wa vituo 10 vya kuchotea maji vya malipo ya kabla. Mradi huo unatarajiwa kunufaisha zaidi ya wananchi 4,715 waishio katika vijiji viwili vya Rahaleo na Mbungulaji vilivyopo katika Kata ya Kalulu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Je, ni lini Serikali itakuwa na mpango maalum wa kubadilisha mita za zamani na kufunga mita za malipo kabla ya matumizi kwenye miradi yote ya zamani ili kuboresha malipo na kurahisisha kwa zile jumuiya za maji?

Swali la pili, mradi huu wa maji wa Kata ya Kalulu ulikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu toka mwaka 2017, huu ni muda mrefu sana mpaka sasa ule mradi haujakamilika.

Je, Waziri anakauli gani ya kuwambia wananchi wa Kalulu kwamba mradi ule utakamilika kwa wakati ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Waziri na kumtua Mama ndoo kichwani? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na pia ninamshukuru Kaka yangu Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya na kuwatetea wananchi wake na hakika pia kuungana na Mheshimiwa Rais kwenye ajenda yake ya kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha kwanza, kufunga *prepaid water meter,* tayari Wizara ya Maji imeshaanza kufunga *prepaid water meter* kulingana na wateja wapya, kwa sababu

hizi ni gharama ambazo zinabebwa na Serikali moja kwa moja, kwa hiyo, tunachofanya ni kwamba, wale wapya tunaanza kuwafungia wanapoomba yale maombi ya kuunganishiwa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kwamba tutaenda sasa kuanza ku-*phase out* zile *mechanical meters* ambazo zilikuwepo hapo kabla, ambazo zilikuwa zinatumika hatua kwa hatua kulingana na fedha ambazo zitakuwa zinapatikana. Lengo kubwa la kufunga *prepaid water meter* tunaamini kwamba kwanza kabisa itapunguza changamoto za bili ambazo zinakuwa zinaleta utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na *predictable* mapato ya hizi jamii zinazohudumia maji *(CBWSO)* na hata mamlaka zingine. Lengo ni kwamba tuhakikishe hatuna malalamiko na mwananchi aweze kujipangia namna gani atumie maji yake. Tunaendelea kulifanyia kazi kulingana na kwamba linahitaji fedha na tutaenda hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya mwaka 2017; imekuwa ni kawaida kwa Serikali kuendelea kuchukua hatua mbalimbali kutekeleza ahadi ambazo zimetolewa na viongozi wetu wa kitaifa akiwemo Mheshimiwa Rais mwenyewe, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, na Naibu Waziri Mkuu. Lengo ni kwamba tunapokuwa tunatekeleza ahadi hizi ni kujenga imani ndani ya Serikali lakini pia ni kuwajengea imani Watanzania juu ya viongozi wao wa kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili suala la Tunduru Kaskazini tumeshalichukua na Mheshimiwa Mbunge alishatueleza mara kadhaa kuhusiana na hili suala. Nikuhakikishie kwamba sasa tunaenda kulifanyia kazi, lakini kipengele cha fedha kitakuwa kinahusika sana ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wake unakuwa wa ukamilifu zaidi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Rungwe, Mji wa Tukuyu ni mji ambao ni sehemu ambayo inanyesha sana mvua lakini tunapata sana shida ya maji. Ni lini Serikali mtawekeza nguvu katika mji huu wa Tukuyu ili wananchi hawa waweze kupata maji kwa sababu wametoka Nyanda za Juu Kusini sehemu zenye mvua nyingi, lakini shida ni kubwa sana ya maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, hakika wakina mama wanaendelea kuonesha juhudi zao za kuwatetea akina mama wenzao katika kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ni kuendelea kuhakikisha kwamba maji juu ya ardhi yanayotokana na mvua, tunajenga mabwawa kama ambavyo sasa tayari tumeshajenga mabwawa 45 na kuna mabwawa takribani 19 yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunakuwa tunatengeneza *catchment* ya maji yasipotee wakati tunajua kabisa kwamba katika maeneo fulani hayana vyanzo vya uhakika vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi kama Serikali tumeshaweka mpango huo, pale ambapo hakuna mito, pale ambapo hakuna ziwa, pale ambapo maji chini ya ardhi ni tatizo tunatumia maji ya mvua na kwa kuyatengenezea mabwawa ili tuweze kuyatumia kwa ajili ya kusambaza maji safi na salama kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, tuko na yeye na yeye tunamuomba kuendelea kushirikiana na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ili kuhakikisha kwamba tunafikisha huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi ya kuuliza swali. Ninaipongeza Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, imetujengea mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kwa kuhudumia Kata za Kashenye na Kanyigo kwa awamu ya kwanza na baadaye awamu ya pili Kata ya Gwanje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo sasa hivi ni takribani mwaka mmoja tangu umefika hatua ya utekelezaji ya 92%; sasa ni nini kauli ya Serikali kuhakikisha mradi huo unakamilika sasa na unawatua wananchi wa Wilaya ya Missenyi katika Kata za Kanyigo na Kashenye ndoo kichwani ili waweze kupata huduma ya maji? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali pia ninapokea pongezi za Mheshimiwa Kyombo, hakika anaendelea kutupatia ushirikiano mzuri na ndio maana anajua hata *progress* ya mradi umefikia asilimia ngapi kwa sababu amekuwa karibu sana na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa mradi huo ni uwekezaji mkubwa sana wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na ametoa fedha nyingi na ndio maana na sisi tunaendelea kuusukuma ili ukamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, tunachokihitaji hata kabla ya mradi haujakamilika kuna *existing infrastructure* ambazo zina uwezo wa kupokea maji kabla ya mtandao mpya haujakamilika. Ninawaelekeza Kagera ili waweze kuangalia namna bora zaidi ya kuanza kutoa huduma ya maji wakati mradi ukiwa unaendelea kukamilika. Nimtoe hofu hilo wataalam wetu watalifanyia utafiti mzuri ili tuweze kufikisha huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmesimama nimewaona, mnaweza mkaendelea kuketi.

Mheshimiwa Deodatus Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, kule Halmashauri ya Mji Njombe tuna mradi mkubwa wa maji unaitwa Igongwi ambao una-*supply* kata tatu. Mradi huu tunamshukuru Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa umekamilika kwa 97% lakini chanzo cha maji kinatoka Ludewa na maji yanapita kijiji kinaitwa Luvuyo na wananchi wa Luvuyo wamezuia mradi huu usikamilike kwa kuruhusu maji yapite kwenye kijiji chao mpaka wao wapate maji.

Nini kauli ya Serikali kuhusiana na kuwasaidia wananchi wa Luvuyo ili wananchi hawa wa kata zile tatu na wenyewe wapate maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na pia ninamshukuru sana Mheshimiwa Mwanyika, Mbunge wa Njombe na naomba kumjibu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sera ya sekta ya maji pale ambapo mradi mkubwa unapita, kushoto kulia kilometa 13 wahusika wanaoishi katika maeneo hayo ni lazima wapate huduma ya maji safi na salama, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, pale kwenye chanzo ambapo tunachukua maji, wananchi wanaoishi katika maeneo ya vyanzo ni lazima wawe kipaumbele kupata huduma ya maji safi na salama. Tunatambua kwamba hata usanifu wetu tunapofanya usanifu wa miradi tunahakikisha kwamba mazingira kama hayo yanakuwa sehemu ya usanifu wetu ili kutoleta changamoto nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunatambua katika mradi huu, katika eneo la Luvuyo ambayo kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, pale kinachoendelea sasa hivi tulishatoa maelekezo kwa *RM* Mkoa wa Njombe kufanya majadiliano ya kina ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaopitiwa na mradi huo wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninatoa maelekezo kwa *RM* Njombe kuharakisha hayo majadiliano ili kuhakikisha sasa tufikie mwisho na hatua zichukuliwe na wananchi wanaopitiwa na mradi huo wapate huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, sisi tushukuru Mji wa Babati upatikanaji wa maji sasa ni 98% lakini tatizo letu ni bili kubwa ya maji. Wananchi wa Babati wanalipa zaidi ya shilingi 1,800 kwa *unit* moja na ninadhani maeneo mengine nchini ni kama 300 au 700. Ni nini kauli ya Serikali juu ya kupunguza bili hizi za maji katika Mji wa Babati kwa sababu wananchi wanashindwa kuzilipia? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Gekul kwa kuendelea kuwapambania Wana-Babati. Ni kweli kabisa gharama za maji inategemea na gharama za uzalishaji na uzalishaji inategemea kwamba ni njia gani iliyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni maji tunayapata kwa njia ya mserereko basi gharama yake itakuwa tofauti, tukipata maji kwa njia ya kutumia umeme wa *solar* maana yake gharama

yenyewe pia itakuwa tofauti, lakini tukipata kupitia umeme wa Gridi ya Taifa gharama yake itakuwa tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, gharama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine inatofautiana kulingana na aina ya uzalishaji. Hata hivyo, uchangiaji wa maji ni suala ambalo hatuwezi kulikwepa iwapo tutazuia au tutapunguza sana gharama za uchangiaji wa maji, maana yake kwamba *sustainability* ya miradi hiyo itafikia kipindi watashindwa ku-*repair* hata vitu vidogo vidogo vitakapokuwa vinaharibika na matokeo yake mradi mzima utakuwa na changamoto ambayo hawataiweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, tunalipokea kama Serikali. Tutatuma wataalamu wetu waende kufanya tathmini na kuangalia gharama za uzalishaji na gharama ambayo tunaifikisha kwa mtumiaji ili tuone kama kuna nafasi ya kupunguza. Serikali haitasita kuchukua hatua ya kupunguza gharama ili mradi Mtanzania apate maji kwa gharama ambayo inakubalika, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eric Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kuniona. Ninaipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa iliyofanyika Buchosa kwenye upande wa maji. Kuna kiasi cha shilingi bilioni 21 zipo kwenye miradi ya maji tayari, lakini ipo changamoto moja kubwa watu wetu Buchosa wanaliwa sana na mamba na maeneo ya Kanda ya Ziwa miradi hii haijafika.

Je, Serikali iko tayari kuongeza *GP* kwenye maeneo kama Maisome, Kanyala, Nyakalilo ili watu waweze kujipatia maji kwa urahisi na kuweza kuokoa maisha yao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Eric Shigongo, Mbunge wa Buchosa kwa kuendelea

kuwasemea wananchi ili kuwaondosha katika hatari ambayo mamba kwa kweli ni Wanyama wakali na wanaweza wakasababisha majanga makubwa na Serikali isingependa kuwaweka wananchi wake katika mazingira ambayo hayana usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni ombi la Mheshimiwa Mbunge na sasa Serikali tunalipokea ombi hili na tutatuma wataalam wetu kwenda kuangalia namna bora zaidi ya kuchukua hatua stahiki ili kuepusha mazingira hatarishi kwa wananchi wetu, lakini pia waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Mheshimiwa Mbunge, Serikali tutaenda kulifanyia kazi kwa uzito stahiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas Zeeland.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, mkandarasi anayejenga mradi wa maji katika Vijiji vya Tandali, Homboza na Mlali amekuwa akisuasua sana kwa kisingizio cha kutokulipwa kwa wakati na mpaka sasa yupo chini ya 60%. Je, nini kauli ya Serikali juu ya kumlipa huyu mkandarasi ili aweze kumalizia miradi hii mikubwa ya maji katika vijiji nilivyovitaja? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Jonas, Mbunge wa Mvomero, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka nilifika Mvomero tukapita katika maeneo na upatikanaji wa maji Mvomero kwa kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan umeongezeka kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunatambua kwamba bado kuna changamoto za hapa na pale, lakini pia tunatambua kwamba wakandarasi wetu wanahitaji fedha ili waweze

kuendelea na miradi. Tayari Waziri wa Maji, amemuelekeza Katibu Mkuu ili waweze kukusanya maombi yote zile hati za madai ili wakandarasi walipwe na waendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna majadiliano na wenzetu Wizara ya Fedha kuendelea kuhakikisha kwamba upatikanaji wa fedha unaendelea kuwepo ili na sisi Wizara ya Maji, tuweze kuwalipa wakandarasi wetu na waendelee na kazi. Nikutoe hofu tutaendelea kulifanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, wakati wa mapokezi ya Mwenge wa Uhuru, ndani ya jimbo langu pamoja na shughuli zingine ulizindua mradi mkubwa wa maji katika Kata ya Michiga ambapo Vijiji vya Michiga, Mnazimmoja na Pachani vitanufaika na mradi huo.

Kwa kuwa mradi ulizinduliwa bila kukamilika kwa 100%; je, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba mkandarasi yule anakamilisha mradi ule kwa wakati ili wananchi wa vijiji husika wakanufaika na mradi huo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Yahya Mhata kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali hairuhusu mradi kuzinduliwa ukiwa haujakamilika kwa 100%, lakini kama kukiwa kuna mazingira ya kuuzindua basi tumeshajiridhisha kwamba, kwanza; kutakuwa na ubora wa maji unaotakiwa na pili; kutakuwa na mazingira ya miundombinu kuwa yamekamilika bila kusababisha upotevu wa maji iwapo yataanza kutumika. Kwa mantiki hiyo na kwa muktadha huo mradi kama umefikia asilimia nzuri kabisa nimtoe hofu, Serikali tupo tayari kumsisitiza mkandarasi akamalizie vipengele ambavyo vinaonekana havijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japo kwa sasa sina taarifa sahihi, lakini ngoja nikitoka hapa nitaenda kulifanyia kazi na nitampa mrejesho Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuona namna gani unakamilika kwa 100%. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, hivi karibuni tumeona miradi mikubwa sana ya maji mbali kutoka katika vyanzo vya maji kama Ziwa Victoria na *Lake Tanganyika,* lakini maeneo ambayo yapo karibu na maziwa au vyanzo hivyo hayana maji.

Je, ni lini Serikali sasa itabadilisha sera hiyo ili maeneo ambayo yapo karibu na hivi vyanzo vya maji yapate maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Kajege na yeye anatoka Kanda ya Ziwa yupo karibu na Ziwa Victoria, ninaamini kabisa kwamba anatamani pia kwamba maji yaweze kumfikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya Serikali ni kuhakikisha kwamba vyanzo vyetu vya uhakika ni maziwa, mito na mara nyingine tunachimba, lakini na maji chini ya ardhi kwa kuchimba visima. Kwa sasa Serikali iliwekeza uwekezaji mkubwa sana kwa Ziwa Victoria na ndio maana maji yakafika Tabora kwa shilingi bilioni 680.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali kupitia mradi wa mabadiliko ya tabianchi ambapo tunayachukua maji Ziwa Victoria kupeleka Nyanshimo, Bariadi, Itilima, Maswa pamoja na Meatu, huo ni mkakati wa Serikali kuendelea kuwekeza, lakini pia sasa tunafanya *feasibility study and details design* kwa ajili ya matumizi ya Ziwa Tanganyika kwa mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa. Lengo ni kwamba tunaenda kutumia vyanzo vyetu vya

uhakika, mito mikubwa kama Malagarasi na maziwa mengine yote ili tuweze kuyatumia kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimtoe hofu, mkakati na sera ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunatumia vyanzo hivyo lakini kwa mazingira ambayo yanaruhusiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaishukuru Serikali kwa kupeleka shilingi milioni 240 Kijiji cha Unyari kumalizia kazi na kumalizia lambo la Mihingo. Wiki mbili zilizopita Mheshimiwa Waziri wa Maji aliagiza mitambo iende Kijiji cha Mkomariro na Kijiji cha Kyandege kuziba lambo la Kyandege na lambo la Mkomariro, sasa mpaka leo ni wiki ya tano hiyo mitambo haijaenda; je, lini mitambo hiyo itaenda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokea changamoto hii kutoka kwa Mheshimiwa Getere na kuona namna gani Waziri wa Maji ameagiza na halijatekelezwa. Ninatoka hapa kwenda kufuatilia utekelezaji wake wa maelekezo ya Waziri wa Maji, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Gitting ilikuwa inategemea maji kutoka vyanzo vya Mlima Hanang. Baada ya maporomoko ya mlima, upungufu wa maji umekuwa mkubwa sana, lakini *survey* imeshafanyika kuchimba visima viwili. Je, lini visima hivyo vitachimbwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa *Engineer* Samweli, ninakumbuka pia tuliweza kutembelea katika maporomoko yale ya Hanang na tuliona namna gani miundombinu ilivyokuwa imeharibiwa, lakini Serikali iliwekeza fedha pale kurejesha ile miundombinu pamoja na kutengeneza njia mbadala ya kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hivi visima viwili ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja, ninaomba nivipokee kwa ajili ya ufuatiliaji tuone kwamba vinaweza kuanza kuchimbwa lini, lakini ninatambua kwamba Wizara ya Maji kupitia bajeti yake ambayo tumeipitisha 2025/2026 inaenda kutatua changamoto ya maeneo ambayo hayana maji kutokana na miradi mikubwa kutopita sasa tunaenda kuchimba visima katika vijiji vingi ambavyo vitakuwa havijapitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu na hivi vijiji viwili vitakuwa sehemu ya utekelezaji wa mradi huo wa uchimbaji wa visima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninataka kufahamu ni upi mkakati walionao kama Wizara kuongeza *flow* ya maji katika Mji wa Isongole kwani maji yapo, lakini kwenye bomba yanatoka kidogo sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *flow* ya maji ni ndogo maana yake *pressure* yake siyo nzuri na kama *pressure* yake sio nzuri kuna mambo mawili yanaweza yakatokea pale. Inawezekana jiografia ya pale inasababisha kuna maeneo mengine maji yanafika yakiwa *pressure* imeshakuwa ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaagiza wataalam wetu wakafanye utafiti pale, wajiridhishe kama tutahitaji kuweka *booster station* katikati ili kuongeza *speed* ya maji kuwafikia wateja basi tutafanya hivyo, lakini kama kutakuwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu ambapo kuna upotevu wa maji sehemu fulani inatokea basi napo tutachukua hatua stahiki kuhakikisha kwamba maji hayapotei yanafika kwa wateja yakiwa na kasi inayotakiwa kwa ajili ya wananchi kuyatumia, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Martha.

Na. 524

**Kumaliza Changamoto ya Maji Maeneo Ambayo Hayana Maji, Sikonge**

**MHE. MARTHA F. MARIKI K.n.y. MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza: -

Je, lini tatizo la maji litamalizwa kwa maeneo yasiyo na mito, mabwawa au mradi wa maji ya Ziwa Victoria hasa Kijiji cha Kiomboi, Kitongoji cha Madole Sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha vijiji vyote vinafikiwa na huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali inatekeleza programu ya uchimbaji wa visima vitano kwenye kila jimbo, hususan kwenye vijiji visivyokuwa na huduma ya maji nchini. Kupitia programu hiyo Kitongoji cha Madole Sita kilichopo Kijiji cha Kiomboi, Wilayani Sikonge kitachimbiwa kisima kirefu, kwa ajili ya kutoa huduma ya maji kwa wananchi wa eneo hilo ambapo kwa sasa kazi ya utafiti wa maji chini ya ardhi inaendelea. Aidha,

Serikali inaendelea na mradi wa utafiti wa maji ardhini na uchimbaji wa visima 17 katika vijiji vyote ambavyo havijafikiwa na huduma ya maji Wilayani Sikonge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Festo.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Katavi una changamoto ya maji kutokana na kuwa na wimbi kubwa la wageni wanaokuja kutafuta fursa mbalimbali za kibiashara. Je, upi mkakati wa Serikali sasa kutoa maji katika Ziwa Tanganyika na kuyaleta katika Mji wa Mpanda ili wananchi wetu waweze kupata maji ya uhakika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, tayari Serikali kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa tumeshaanza kufanya *survey* ili kuhakikisha tunahitaji fedha kiasi gani, lakini pia kuna maeneo mengine ambayo tayari wameshaanza kutumia maji ya Ziwa Tanganyika. Kwa upande wa Katavi bado hatujaanza kutumia maji hayo, lakini kuna miradi mikubwa inaendelea katika Mji wa Mpanda na kuna Mradi wa Miji 28 unaendelea, ambapo ukishakamilika upatikanaji wa maji ni zaidi ya 80%, kwa upande wa Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na Serikali itaendelea kuharakisha kufanya *feasibility study and details design,* ili kuhakikisha tuna-*establish* gharama ambazo zitahitajika kwenda kujenga mradi huo na wananchi waanze kufaidika na maji ya kutoka Ziwa Tanganyika, hasa Mkoa wa Rukwa, Katavi na Kigoma, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kuwa katika taasisi za elimu, hasa shule za sekondari na msingi, hazina maji ya uhakika. Aidha, kutokana na wakati mwingine bili kuwa kubwa wanashindwa kulipa.

Je, hawaoni kwamba, ni muda muafaka sasa kuwachimbia visima katika maeneo hayo, hasa zile shule ambazo zinasuasua katika ulipaji wa bili, ili wawe na maji ya uhakika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ni lengo la Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba Watanzania wanaweza kuwa na *accessibility* ya maji, na maji hayo yawe *affordable,* safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ambayo tutachimba visima pale ambapo tukipima na kujiridhisha maji chini ya ardhi yanapatikana na pale ambapo tutajiridhisha maji chini ya ardhi hayapatikani, tutafanya *extension* ya miradi iliyopo pale karibu. Gharama hazitakwepeka kwa baadhi ya maeneo, lakini kuna maeneo ambapo tutakapoweza kuchimba visima tunaweza kukwepa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika usanifu wa miradi mikubwa tumeendelea kutoa kipaumbele kwenye taasisi za umma; zahanati, vituo vya afya na pia shule za msingi na sekondori. Lengo ni kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapokuwepa shuleni wawe na uhakika wa kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama kubwa za maji zitasababisha baadhi ya shule kushindwa kulipia na ukishindwa kulipia matatizo yatarudi kwa watoto wetu ambao wapo katika shule hizo. Tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa Ilemela, mahiri kabisa, tutaendelea kuufanyia kazi na kuchakata kuona ni kwa namna gani tunashirikiana na Ofisi ya Rais,

TAMISEMI, kuja na mkakati mzuri zaidi wa kutatua changamoto hii kwa muda ambao unakuja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nini mpango wa Serikali kwa maeneo haya ambayo yana ukame kutengeneza pesa maalum, kwa ajili ya mabwawa kama Kiteto hivi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, arudie kidogo swali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edward, uliza kwa Kiswahili, siyo kwa Kimaasai, tafadhali. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa kuwa maeneo mengi kuna ukame na kuna uhitaji mkubwa sana wa mabwawa kama Kiteto. Nini mpango wa Serikali kutafuta pesa maalum kwa ajili ya kujenga mabwawa Kiteto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Olelekaita, Mbunge wa Kiteto kwa kuendelea kuwa mshauri mzuri katika sekta yetu ya maji pale ambapo tutakuwa tunahitaji, lakini pia kwa kuendelea kutoa maoni ya namna gani tunaweza tukaboresha zaidi katika kutatua huduma ya maji nchini, hasa katika maeneo yenye ukame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimesema hapo awali Serikali tayari imeshaanza kujenga mabwawa mengi tu ya kutosha katika maeneo ambayo yana ukame na tunafahamu kwamba maendeleo ni hatua kwa hatua. Kama ambavyo tumeshakamilisha mabwawa 45 na mabwawa 19 yakiwa katika

hatua mbalimbali za utekelezaji, tunaendelea kufanya tathmini pale ambapo yanakuwa yamebaki tunahitaji kiasi fulani, ili tuweze kuweka mkakati maalum wa kupata hizo fedha kwa ajili ya mabwawa ambayo yataenda kutosheleza katika maeneo mengi yenye ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mabwawa peke yake hayatakuwa suluhisho la kudumu katika baadhi ya maeneo, na ndiyo maana maeneo kama ya Tabora, ilionekana kabisa upatikanaji wa maji chini ya ardhi ulikuwa ni tatizo kubwa. Ndio maana Serikali ikaweka shilingi bilioni 680 ikafikisha pale, ikaweka shilingi bilioni 143 Sikonge, Kaliua na Urambo, lakini pia imeendelea kufanya *extension* Igunga shilingi bilioni 22. Mambo haya yanafanyika kwa sababu Serikali ina dhamira ya dhati kabisa ya kuhakikisha kwamba wananchi wake, haijalishi wapo katika maeneo gani, wanapata huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza. Mheshimiwa Mbunge tumepokea ushauri wako tutaufanyia kazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, sasa aulize swali lake.

Na. 525

**Changamoto ya Maji, Kata za Mwananyamala na Makumbusho**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza: -

Je, nini kauli ya Serikali juu ya changamoto ya maji maeneo ya Jimbo la Kinondoni hususani Kata za Mwananyamala na Makumbusho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha maeneo yote ya Jiji la Dar es Salaam yanapata huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza, zikiwemo Kata

za Mwananyamala na Makumbusho. Kata hizo zimekuwa na ongezeko kubwa la watu huku miundombinu yake ya maji ikiwa ni ya muda mrefu na inakabiliwa na changamoto ya uchakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 itakarabati miundombinu ya maji katika eneo la Kisiwani Msikitini, kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo yote ya Kata za Mwananyamala na Makumbusho, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Bunge hili wakati wote linafahamu juu ya juhudi ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba maji yanapatikana kwa wananchi wa Tanzania. Mheshimiwa Waziri anasema matatizo haya ya Mwananyamala na Makumbusho yatatatuliwa mwaka wa fedha ujao, 2025/2026. Maji siyo kama umeme kwamba unaweza ukawasha kibatari, ni lazima upate maji sasa.

Swali langu ni, hawa wananchi watakaa hivyo mpaka mwaka wa fedha unaokuja, ambao tarehe haijulikani, wanakwenda kupata kwa njia gani? Swali langu hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, changamoto hii sasa imekuwa hadi kufikia Mtaa wa Hananasif katika Kata ya Hananasif, ina maana matatizo yanaendelea kuwa mengi.

Swali langu, *DAWASA* inafanya biashara, hivi mnataka kutuambia sisi Wabunge kwamba *DAWASA* inashindwa kupata fedha hata za kukarabati miundombinu ambayo inaifanya maji yaweze kupatikana na wao waweze kuyauza hayo maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Tarimba Abbas, Mbunge wa Kinondoni na tunamshukuru sana kwa kuendelea kuishauri

Serikali katika sekta hii ya maji na sisi Serikali kupitia kwa wataalamu wetu tumekuwa tukipokea maoni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mwananyamala na Makumbusho ni lazima kuwepo na mabadiliko ya miundombinu ambayo ilikuwa inatoa huduma ya maji. Uchakavu wake unaweza kuwa ni tatizo lingine pia, lakini kikubwa ni maji kutopatikana katika maeneo haya siyo tu kwa sababu ya uchakavu wa miundombinu, Jiji la Dar es Salaam wakazi wanapoingia na kutoka, wanapojenga na kubomoa, inatuathiri hata sisi katika miundombinu yetu ya maji. Kwa hiyo, kwa muktadha huo tatizo na changamoto ya miundombinu kwa upande wa Dar es Salaam kwa kuangalia jiografia ya ujenzi wa wake haitakwepeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa ni Serikali inatambua changamoto hiyo inayotokana na mazingira kama hayo na tumekuwa tunachukua hatua kulingana na aina ya changamoto iliyojitokeza. Lengo kubwa la Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la ujenzi wa miundombinu chakavu, urekebishaji au uboreshaji unatokana bajeti ambayo tunaipitisha hapa Bungeni. Kama Serikali, si vyema sana tukawa tunatoa ahadi za uongo ambazo hazitaweza kwenda kutatua changamoto zaidi ya kuanzisha taharuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge katika bajeti ya 2025/2026, kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi, tutaenda kufanyia kazi eneo la Msikitini ambalo ndilo litaenda kusaidia upande wa Makumbusho pamoja na Mwananyamala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa *DAWASA;* hata gharama ambazo *DAWASA* anatoza, ukiangalia *production cost* ya *DAWASA,* ulipaji wa kemikali, watalaam wake kuzunguka kuangalia na kutathmini changamoto zilizopo, ni kweli kabisa kwamba tunaweza tukasema ni rahisi sana kupata mapato na

kuanza kuyawekeza katika uboreshaji wa miundombinu, lakini gharama za uendeshaji ziko juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama yake haijapitiwa takribani miaka sita ambapo hapa katikati kumekuwepo na mabadiliko ya dola na hizi kemikali tunazipata kutoka nje ya nchi, vipuri tunavipata kutoka nje ya nchi ambapo kuna mabadiliko, lakini gharama ya *DAWASA* bado imebaki ileile kiasi kwamba ni mzigo mkubwa. Ni lazima tuseme ukweli inapofikia kusema ukweli, lazima tuone namna gani ya kuisaidia *DAWASA* na kupitia bajeti hii ambayo tumeipata naamini kabisa kwamba tutaweza kwenda kutatua baadhi ya changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, kupitia kanuni ambazo zinaongoza Mfuko wa Taifa wa Maji, sasa 29% inaenda kusaidia ku-*subsidize* zile mamlaka zetu pale ambapo hawana uwezo wa kufanya jambo kupitia Mfuko wa Maji, yale makusanyo yake yataenda kusaidia ku-*subsidize,* lengo ni kwamba mamlaka hizi zisije zikakumbana na tatizo la kutotoa kabisa huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea ushauri wake na tutaendelea kuufanyia kazi, lakini ni vizuri pia, tukatoa taarifa Watanzania wafahamu gharama ya uzalishaji wa maji ni kubwa sana, hasa kwa Jiji ya Dar es Salaam, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza, nakupongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali na pia naipongeza Serikali ya mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo imekuwa inashughulikia changamoto kubwa hii ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kishapu bado tuna changamoto ya zaidi ya kata tisa ambazo hazina maji. Nataka nipate majibu, ni lini sasa Serikali itapeleka maji katika Kata ya Shagihilu, Ndoleleji, Masanga, Mwamalasa na

Somagendi ambazo zina changamoto kubwa sana ya maji? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Butondo, Mbunge wa Kishapu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi ambapo Kishapu imebadilika kwa kasi sana katika sekta ya maji ni hiki cha 2020 – 2025. Upatikanaji wa maji kupitia bomba la kutoka Ziwa Victoria na ile *extension* yake umesaidia sana kupunguza makali ya ukosefu wa huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba ni kata hizi tisa ambazo Mheshimiwa Butondo ameendelea kuzipambania na sisi Serikali, tumeshasikia kilio cha Wana-Kishapu kupitia kwa mwakilishi wao mahiri kabisa. Wizara ya Maji katika bajeti iliyopitishwa ya shilingi trilioni 1.061, tunamhakikishia kwamba, hizi Kata tisa tunaenda kuzifanyia kazi na wananchi wa Kishapu watapata huduma ya maji safi na salama, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daimu Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, *RUWASA* Wilaya ya Tunduru, walifanya upembuzi yakinifu wa mradi wa maji katika Mji Mdogo wa Nalasi, wenye vijiji vinne vya Lipepo, Nalasi, Chilundundu Kusini na Chilundundu Kaskazini. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kutekeleza mradi ule? *(Makofi)*

**MHE. MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninamshukuru sana kaka yangu kwa kazi nzuri na vile vijiji vinne kwa kweli, najua ni kipaumbele chako Mheshimiwa Mbunge na hakika unajua kwamba, eneo lile lina wakazi wengi ambao ni wapiga kura wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wapiga kura wako na Madiwani pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofanya upembuzi yakinifu hatua inayofuatia ni Serikali kupata fedha, kwa ajili ya kupata usanifu wa kina. Baada ya kufanya usanifu wa kina ndio tujue mradi huo utagharimu kiasi gani na baada ya kujua ndio utengewe fedha hiyo, kama haipo itafutwe, ili sasa twende kutekeleza mradi huo wananchi wa kata hizo nne waweze kupata huduma ya maji, safi na salama, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, nakuruhusu.

Waheshimiwa Wabunge, leo tuna wageni wengi kidogo na naomba mniruhusu niwatangaze waliopo, halafu tuwaruhusu waweze kuwapisha wageni wengine.

Tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni wageni nne wa Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Mbunge na Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, hawa ni wajukuu wa Samia kutoka Jijini Dar es Salaam. Naomba niwatambue kwa majina; kwanza tuna Ndugu Emmanuel Lema *(Boss Kimaro),* naomba usimame; tunaye Ndugu Tausi Mdegela; naomba wote msimame kwa pamoja na Meya Shabani *(Mr. Pimbi)*. Huyu Meya Shabani ni *Mr. Pimbi,* nadhani ni jina lake hilo. *(Makofi)*

Ndugu Tausi Mdegela ambaye ni maarufu kama Tausi; tunaye Ndugu Latifa Kasanga; hawa wote ni wasanii wa michezo ya kuigiza, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tuna wageni 50 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni wanamichezo wa *Mandela Veteran Sports Club* kutoka Songea Mjini, Mkoa wa Ruvuma; wazee wa *Veteran,* karibuni ma-*veteran* wetu. *(Makofi)*

Jamani hawa ni *Mandela Veteran Sports Club* kutoka Mji wa Machifu, pale Songea Mjini, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 14 wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Mbunge ma Waziri wa Madini ambao ni Taasisi ya *Tanzania Medical Students Associations (TAMELISA)* kutoka Jijini Dodoma. Kama wapo, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 20 wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge na Naibu Waziri wa Madini, hawa ni Kwaya ya Mt. Mikael Malaika kutoka Parokia ya Mt. Josephine Bakhita Korona ya Njiro, Mkoani Arusha, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge ambaye ni Ndugu Tumaini Mtatuu, huyu ni rafiki yake na ni Muuguzi kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge ambaye ni Mheshimiwa Bahati Sebastian Mamboma, Diwani wa Kata ya Kibosho Kati na Katibu wa Madiwani, Manispaa ya Moshi, karibu sana. *(Makofi)*

Nadhani ni kupitia Chama Cha Mapinduzi, bila shaka, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge ambao ni familia ya Mheshimiwa Hamidu Selemani Said, Diwani wa Kata ya Mirongo kutoka Nyamagana, Jijini Mwanza, karibu sana, popote mlipo, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge ambao ni ndugu zake kutoka Kishapu, Mkoani Shinyanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Lubala Mabula, Mbunge, ambaye ni mwalimu Buchadi Juvenalis kutoka Shule ya Amani Nzali, Wilaya ya Chamwino, Mkoani Dodoma, hatujamwona, ahaa, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge ambao wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 78 wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge ambao ni wanafunzi 71 na walimu saba wa Shule ya *St. Getrude* kutoka Mkoani Pwani, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kwanza tunaye Ndugu Marystella Medard kutoka *Area A*, Jijini Dodoma, karibu. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Hansen Turuka wa Shule ya Sekondari Rosmin kutoka Mkoani Tanga, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 76 na walimu sita kutoka Shule ya Msingi *Lady of Mercy* iliyopo Suye, Jijini Arusha, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 30 na walimu watano wa Shule ya Awali na Msingi *Bible Baptist Academy* kutoka Jijini Arusha, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Mwisho tunao wanafunzi 66 na walimu sita kutoka Dawati la Elimu Shule ya Msingi Yerusalem iliyopo Mbezi Beach, Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bunge; tumefurahi kuwaona. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, wale wanaohusika na wageni wataendelea kutupa utaratibu kadri tutakavyoona inafaa.

Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na hapa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 526

**Kumaliza Migogoro ya Wafugaji na Wakulima – Morogoro**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza migogoro ya wafugaji na wakulima Mkoani Morogoro?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwepo kwa migogoro ya wafugaji na wakulima Mkoani Morogoro. Hata hivyo, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana na migogoro hiyo ambapo baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi za vijiji ili kubainisha maeneo ya kilimo sambamba na maeneo ya wafugaji kupitia Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi. Aidha, hatua nyingine ni kupitia Mradi wa KKK ambapo miji chipukizi kama ilivyo kwa miji ya halmashauri kupangwa, kupimwa na kumilikishwa sambamba na kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa wananchi kuhakikisha kuwa wanatumia ardhi kuendana na mipango ya matumizi iliyopangwa ili kuondoa muingiliano wa matumizi ya ardhi ambayo imekuwa ni chanzo cha migogoro ya wakulima na wafugaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza kabisa ninashukuru kwa majibu mazuri sana ya Naibu Waziri ambayo pia yanaridhisha, lakini nina maswali mawili ya ngongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza; Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi katika Mkoa wa Morogoro ulianzishwa katika baadhi ya wilaya zikiwemo Wilaya za Manyinyi, Ulanga, Kilombero, Kilosa pamoja na Mvomero; lakini kilichotokea ulisimama; je, ni lini mpango huu utaendelea kusudi wakulima na wafugaji waweze kuishi vizuri?

Swali langu la pili, je, kuna mkakati gani wa kutoa elimu kwa wote hasa kwa wakulima na wafugaji ili waweze kuishi kwa kutegemeana? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nimshukuru sana Dkt. Christine Gabriel Ishengoma kwa maswali yake mawili ya nyongeza; kwamba je, lini mpango huu utaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa sasa hivi baadhi ya wilaya tunaendelea nazo baada kupata fedha kidogo kutoka Serikalini na muda mfupi ujao baada ya kuwa mmetupitishia bajeti tutakapokwenda kuanza mwaka mpya ya fedha, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hili litakuwa linakwenda tena kuanza na kumalizia maeneo yaliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu, hili ni lazima wote tusaidiane kwa sababu katika uhalisia, Wizara imeendelea kutoa elimu katika maeneo mbalimbali. Peke yake haitoshi, niwaombe na wenzetu TAMISEMI ambao ndiyo wanaosimamia namna bora ya matumizi bora ya ardhi kwenye maeneo hayo wazingatie yale maeneo ambayo yametengwa na wananchi wapate elimu ya kutosha ili muingiliano ule usiwepo mkubwa hata kusababisha mgongano wa wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe wasiwasi tu Wizara inaendelea kutoa elimu kupitia redio, *television,* lakini kupitia mikutano ya hadhara na makongamano kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi kujua umuhimu wa namna bora ya kutumia ardhi tuliyonayo ambayo kama nilivyosema huko awali

hatuna mbadala wala hatuna namna tutakavyoweza kuiongeza ardhi hii tuliyonayo ambayo ni ya urithi wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi yaani katika kila mikoa inaendelea na ipo; je, Wizara ya Ardhi hawaoni kwamba ipo haja sasa ya kuwatumia wanafunzi wanaotoka Tabora pale Ardhi pamoja na wanafunzi hawa wa Ardhi, Dar es Salaam wakafanya hiyo kampeni ya kumaliza hii migogoro, kwa sababu wale watoto wapo na na wengi, wakafanya hiyo angalau kwa miezi sita mkamaliza haya matatizo? Ahnsate.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nipende kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ntara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba migogoro hii tumeendelea kuipunguza kwa kasi kubwa sana na yeye mwenyewe atakubaliana na mimi kuwa wale wanafunzi wa vyuo hivi tumeendelea kuwatumia na si kwamba hawatumiki. Wametumika katika miradi mbalimbali, na hasa hii ya kwenda kubainisha matumizi bora ya ardhi katika maeneo mbalimbali. Walikwenda mpaka mikoa kadhaa na wametusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza kabisa katika kumaliza migogoro hii ni wananchi wenyewe kutambua namna ya kutumia rasilimali ardhi waliyonayo katika kuzingatia yale matumizi waliyojipangia wao wenyewe. Hii itatusaidia sana kupunguza mgongano huu wa kimaslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa wenzetu ambao ni wafugaji, sasa kuwa na ufugaji wa kisasa utakaokuwa unazingatia mazingira halisi ya thamani ya mifugo yao badala ya sasa

ambapo wamekuwa wakifugia kama vile desturi, mila na kama *hobby* hivi ya ufugaji. Sasa matokeo ya wafugaji hawa bado hayajaweza kuwa na mchango mkubwa katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo turudi kwenye uelewa wa pamoja, kwamba tuwe na ufugaji bora wenye malengo sahihi kabisa ya kuleta maendeleo kwenye jamii husika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na migogoro ya ardhi kati ya wawekezaji na wananchi katika Mkoa wa Kilimanjaro, hasa Jimbo la Moshi Vijijini, na imeonekana kuleta athari hasi kwa muda mrefu kwa sababu migogoro hii imedumu kwa muda mrefu bila suluhisho; je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wanakwenda kutatua migororo hii ili wananchi waweze kuishi kwa amani? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ufupi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kimsingi Mbunge wa Jimbo hili amekuwa karibu sana na sisi kwa ajili ya kufuatilia namna ambavyo tunaweza kwenda kuimaliza hii migogoro. Tunakumbuka kuna baadhi ya migogoro ambayo tayari tulishakutana na Mheshimiwa Mbunge, tumemwelekeza namna ya kwenda kulimaliza suala hili, na tunapata ushirikiano mkubwa sana kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo. Mimi nikuhakikishie tu Mheshimiwa Njau ukishirikiana vizuri na Mheshimiwa Mbunge wa jimbo…

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba anijibu swali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** …mtaelewa namna ambavyo tunashughulikia masuala haya.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Angeline Silvester Lubala Mabula, Mbunge wa Ilemela aulize swali lake.

Na. 527

**Ujenzi wa Kiwanja cha Michezo Manispaa ya Ilemela**

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa kiwanja cha michezo *(centre of excellence)* Manispaa ya Ilemela chenye hekari 16.75 ambacho kina hati tayari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina dhamira ya dhati ya kuendeleza eneo hilo. Hata hivyo kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele katika kukamilisha miradi ya ujenzi wa miundombinu ya michezo ambayo itatumika kuendeshea mashindano ya *CHAN 2025* na *AFCON 2027*. Aidha, Serikali imeanza ujenzi wa akademia ya michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kilichopo Wilaya ya Kwimba, mkoani Mwanza ambapo utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 25.4. Hivyo kwa kuanzia, wananchi wa Mkoa wa Mwanza watanufaika na mradi huo mara utakapokamilika, huku tukiendelea kujipanga na utekelezaji wa mradi katika Manispaa ya Ilemela.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais ambaye amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha michezo inainuka na tumepata pia fursa ya kuwa wenyeji wa michezo ya *AFCON*. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua dhamira njema ya Serikali ya kutaka kuendeleza michezo hasa kwa kuwa na hizi akademia za michezo, mojawapo hiyo ya Malya ambayo ameitaja; je, haoni kwamba kutoanza kujenga ule uwanja ambao tuliambiwa ungeweza kuanza mwaka huu wa Ilemela ni kuwavunja moyo wananchi wa Ilemela ambao walitoa kile kiwanja chao bure kwa Serikali bila masharti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika viwanja vitano ambavyo vilitajwa kama kuwa wenyeji wa michezo ya *AFCON*, uwanja wa CCM Kirumba nao ulitajwa; je, ni lini Serikali itaanza ukarabati wa uwanja ule ili kuwa tayari kutumika kwa michezo ya *AFCON 2027?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula kwa ufuatiliaji mzuri wa masuala ya Wana-Ilemela ikiwamo ufuatiliaji kwenye masuala ya michezo na hasa kituo hiki ambacho ameuliza swali lake la msingi leo; ninaamini Wana-Ilemela wanaliona hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maswali yake mawili ya nyongeza, kwanza kuhusu kuchelewa kuanza kwa kituo hiki cha Ilemela; kama ambavyo nimejibu katika wakati najibu swali la msingi, sasa hivi *emphasize* ipo katika ujenzi wa miundombinu itakayotumika kwa ajili ya *CHAN* 2025 na *AFCON 2027*. Kituo hiki kipo katika mipango ya Serikali, hatujakiondoa na tunamwomba Mheshimiwa Mabula kwa niaba ya Wana-Ilemela waendelee kuwa na subira, tutakapomalizana na miundombinu kwa ajili ya

*CHAN 2025* na *AFCON 2027* tutahamia kwenye ujenzi wa vituo mbalimbali kikiwemo Kituo cha Ilemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimtoe wasiwasi, Serikali bado ina mpango nacho kituo hiki na itakifanyia kazi kadri hali itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na viwanja vitano ambavyo vilikuwa vimetengwa kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati, kwanza viwanja hivi vitano havitatumika moja kwa moja kwa ajili ya *AFCON*, viwanja vitakavyotumika itakuwa ni uwanja Benjamin Mkapa Dar es salaam, uwanja mpya unaojengwa Arusha na uwanja wa Amani Zanzibar. Viwanja hivi vitano tulikuwa tunavikarabati kwa ajili ya kuvifanya kama *backup* na uwanja wa CCM Kirumba ni miongoni mwa viwanja hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimtoe wasiwasi, mpango huu upo pale pale na tupo katika mazungumzo ambayo yapo katika hatua iliyosogea sana na mmiliki wa viwanja hivi ili kuona utaratibu bora wa kuvifanyia ukarabati, matumizi yake kwa maana ya uendeshaji na namna ambavyo thamani ya fedha ya umma itakayotumika kwenye ukarabati wa viwanja hivi itakavyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimtoe Mheshimiwa Mabula wasiwasi, uwanja wa CCM Kirumba bado upo katika mipango ya Serikali na hivi karibuni tutaanza ukarabati wake kama ambavyo tutaanza kwenye viwanja vingine vinne ambavyo vinakwenda kuungana na CCM Kirumba kwa ajili ya *backup* ya michezo ya *AFCON 2027*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Maswali yawe kwa ufupi sana na majibu yawe kwa ufupi kadri itakavyowezekana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Esther Matiko, atafuatia Mheshimiwa Abubakari Asenga na Mheshimiwa Yustina Rahhi.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mkoa wa Mara ni mkoa ambao anatoka muasisi wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, lakini Mkoa wa Mara hauna

uwanja wa mpira wenye hadhi ya kimataifa. Kwa kuwa uwepo wa uwanja huu ungeweza kutoa fursa mbalimbali kama ajira, kukuza utalii, maana tuna Mbunga ya Serengeti na kule Butiama kwa Baba wa Taifa na baadaye kukuza uchumi wa nchi yetu.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kuweka katika mpango wake ujenzi wa uwanja wa mpira wenye hadhi ya kimataifa na kulipa jina Mwalimu Nyerere katika Mkoa wetu wa Mara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Esther Matiko; anayo hoja kimsingi na Serikali inaona haja ya kuwa na viwanja na miundombinu mbalimbali ya michezo nchi nzima. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ya kwamba tunaingiza katika mpango wa Serikali wazo lake na tutalifanyia kazi kadri rasilimali fedha itakaporuhusu na wakati utakapokuwa rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni wazo zuri na mimi namuunga mkono ya kwamba ni muda wake sasa wa kufanyiwa kazi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Ifakara Jimbo la Kilombero ni halmashauri inayokua kwa kasi sana na ina vipaji vingi sana vya vijana vya michezo; mfano Aishi Manula anatoka Kilombero na tuna maeneo mengi sana ya ujenzi wa viwanja vya michezo, mfano eneo ambalo lipo karibu na Kituo cha Afya cha Kibaoni pale Ifakara, Mwaya na CCM kwa Tangani.

Je, ni lini Serikali itafanyia kazi ombi letu la kujenga uwanja wa kisasa wa michezo katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara ili kuendelea kukuza vipaji vya vijana wetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Asenga kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuhakikisha masuala mbalimbali ya wanajimbo la Kilombero hayafumbiwi macho, yakiwemo masuala katika sekta ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika maswali yaliyotangulia, lengo la Serikali na lengo la Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na miundombinu bora ya michezo nchi nzima ili kuweza kugundua vipaji na kuvilea na kuhakikisha vijana pengine wanakutana na riziki alizowaandikia Mwenyezi Mungu kwa kutumia vipaji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Asenga, kwa sasa Serikali inafanya kila inaloweza kuhakikisha kwamba miundombinu kwa ajili ya *CHAN* 2025 na *AFCON 2027* inakamilika, hali kadhalika Serikali inaunda mamlaka ya usimamizi wa miundombinu ya michezo ambayo itakuwa inaitwa *SIMA* ili kwenda kutekeleza kwa vitendo maono ya mwanamichezo namba moja wa nchi hii, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Miongoni mwa mambo ambayo itayafanya ni kuhakikisha tunakuwa na miundombinu bora ya michezo katika nchi nzima; na Jimbo la Kilombero halitoachwa nyuma. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yustina Rahhi.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga uwanja wa mchezo katika Wilaya ya Mbulu ambapo ni eneo muhimu sana kukuza vipaji vya riadha; tukizingatia kwamba wanariadha mashuhuri kina John Steven wametokea eneo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na swali zuri la Mheshimiwa Yustina, ni kweli kwamba vipaji vingi vya riadha vinatokea katika ukanda anapotokea Mheshimiwa Mbunge na tumeweza kuona, faida kubwa imepatikana kwa wanariadha na medali nyingi ambazo wameshinda wakati wakiliwakilisha Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali bado ina mipango ya kuendelea kujenga miundombinu mbalimbali ya michezo na sasa hivi tumejenga kituo cha michezo katika ukanda huu wa eneo la Karatu. Hii ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunavigundua na kuvilea vipaji hivi anavyovitaja Mheshimiwa Mbunge na kadri hali itakavyoruhusu tutafika chini zaidi na kuhakikisha kwamba tunajenga kituo cha michezo kwenye eneo analolitaja Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Mji wa Kahama ni mji ambao unakua sana na unakua kwa kasi na una vitu vingi vizuri na una vipaji vya watoto wa kike ambao wanacheza mpira wa miguu, lakini hakuna uwanja.

Je, nini kauli ya Serikali au mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Kahama inapata uwanja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefika Kahama na Mheshimiwa Mnzava analifahamu. Ni kweli Mji wa Kahama unavyo vipaji vingi na mji unakua kwa kasi sana. Kwa sasa kama ambavyo nimetangulia kusema msisitizo uko kwenye viwanja ambavyo vitatumika kwa ajili ya *CHAN* na *AFCON* na nitoe rai kwa mamlaka husika za Wilaya na Mji wa Kahama kuhakikisha kwamba wanatenga fedha kutoka kwenye mapato yao ya ndani ili kuanza kutengeneza miundombinu bora ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara nimhakikishie kuwa tuko tayari kutoa usimamizi wa kitaalamu kuhakikisha tunawaunga mkono na hali ya rasilimali fedha itakaporuhusu, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutawaunga mkono kwa kuhakikisha tunawasaidia kukamilisha miundombinu hiyo ya michezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, niliwahi kuuliza na ninakumbusha kwamba ni lini Serikali itachukua sehemu ya mapato yanayopatikana wakati klabu kubwa za mpira kama Simba na Yanga zinapocheza na kupeleka maeneo ya pembezoni ambako kuna wapenzi wengi na hawana viwanja vya mpira? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninalikumbuka swali hili la Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mbunge, bado tunapata wakati mgumu wa kuona namna ambavyo tunaweza tukachukua mapato haya na kuyapeleka katika sehemu ambayo Mheshimiwa Mbunge anataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ambayo yanapatikana kwenye michezo ambayo klabu hizi zinacheza bado ni makubwa sana mpaka sasa hivi na tunaangalia namna ya kuyapunguza ili klabu hizi ziendelee kunufaika ama zinufaike zaidi. Kwa hiyo, utakapofika wakati ambapo tunawakata zaidi sasa kwa ajili ya kupeleka kwenye miundombinu ya michezo kwa sehemu za pembezoni, ninafikiri kutaleta malalamiko makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho tunajaribu kufanya sasa hivi ni kuhakikisha Serikali inaendelea kutenga asilimia tano kutoka katika michezo ya kubahatisha ili kuhakikisha kwamba tunafanya shughuli mbalimbali za maendeleo ya michezo zikiwemo ambazo Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya

amezitaja, lakini kwenye kuzikata *club* ninafikiri kwa sasa itakuwa ngumu. Siyo jambo ambalo linaweza kuongeleka kirahisi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante.

Tunaendelea na swali linalofuata, Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 528

**Upotevu wa Fedha za Umma kwa Kukosa Mifumo Madhubuti**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza: -

Je, Serikali imepoteza fedha kiasi gani mwaka 2015 - 2020 kwa kutokuwepo usalama madhubuti wa mifumo ya usimamizi kufuatia mabadiliko ya TEHAMA? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Fedha, karibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mabadiliko ya TEHAMA yametumika kama fursa ya kujenga mifumo yetu wenyewe ya kukusanya mapato na kudhibiti matumizi. Mifumo hiyo imeiwezesha Serikali kukusanya mapato kwa ufanisi na hivyo kudhibiti kiwango cha uvujaji wa mapato kilichokuwepo kutokana na kutotumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato. Kwa mfano, mara baada ya kuanza kutumia mfumo wa kukusanya mapato wa *GePG,* mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, idara na taasisi yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 689 mwaka 2014/2015 hadi kufikia shilingi trilioni 2.21 mwaka 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la takriban 400%.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali, wamesema wamekusanya shilingi bilioni 689 tangu mwaka 2014/2015 mpaka 2019/2020 kutoka shilingi bilioni 689 mpaka shilingi trilioni 2.21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia majibu ya swali na swali nililouliza, swali langu halijajibiwa, ila sasa ninajua kuna *ethics* za kutoa taarifa za mifumo. Ninajua ni taarifa *sensitive* na ndiyo maana hawajazisema. Wao wanasema kuna ongezeko la 400% na nimesema ninawapongeza, lakini mimi nimetaka kujua mpaka sasa tumepoteza fedha kiasi gani?

Kwa hiyo, ninatambua kwamba inawezekana ni taarifa ambazo ni nyeti hawajazitoa, kwa hiyo hata tukilirudisha halitajibiwa. Mimi sitakuwa na maswali ya nyongeza, lakini ninaomba tu tukubaliane kwamba kuna shida kubwa kwenye mfumo. Kuna upotevu wa fedha na ripoti ya *CAG* inaonesha kwamba kuna upotevu mkubwa wa fedha... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Hanje...

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niombe tu, *commitment* ya Serikali kwenye hili ya dhati kabisa, wahakikishe wanatumia teknolojia zote zilizopo duniani na mapinduzi makubwa ya sasa ya kiteknolojia duniani...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kuhusu utaratibu tafadhali. Ninaomba uketi…

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** …kudhibiti mfumo wa upotevu wa fedha kwa sababu zinapotea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ninaomba uketi. Mheshimiwa Nusrat Hanje, ninajua utaratibu unaufahamu.

Waheshimiwa Wabunge, ninadhani swali liko wazi. Linasema, je, Serikali imepoteza fedha kiasi gani tangu mwaka 2015 mpaka 2020 kwa kutokuwepo usalama madhubuti wa mifumo ya usimamizi kufuatia mabadiliko ya TEHAMA duniani? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa uelewa wangu, ili swali hili lijibiwe lazima liwe linalinganisha. Sasa majibu wa Serikali hapa yalipo kwa namna swali lilivyoulizwa, yanajitosheleza kwa sababu swali lipo na majibu yapo hapa kwa maandishi. *Unless,* Mheshimiwa Nusrat Hanje ungependa majibu mengine. Ninaomba nitoe tu maelekezo kwamba unaweza ukaandika upya swali lako kwa kulingana na majibu ambayo unayatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, ninakuruhusu urejee au kama kuna swali la nyongeza? Ninadhani hakuna kwenye eneo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Viwanda na Biashara, samahani sio Viwanda na Biashara, tunaendelea na Wizara ya Fedha hiyo hiyo na ni swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 529

**Kampuni za Ndani Kupewa *Tender* za Bilioni 50**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza: -

Je, nini mkakati wa kuzijengea uwezo kampuni za ndani kuzipa *tender* za shilingi bilioni 50 kwani sheria ya manunuzi inaruhusu kupewa *tender* za shilingi bilioni 20?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kifungu cha 57 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 10 ya Mwaka 2023 na kanuni ya 45 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 zimetenga zabuni za hadi shilingi bilioni 50 kwa ajili ya wazawa na kampuni za ndani. Utekelezaji wa sharti hili la sheria linatekelezwa kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma *(NeST)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kifungu cha 61 cha sheria hiyo, kinaelekeza watu au kampuni binafsi kama hazina uwezo wa kutekeleza mikataba kuingia katika ushirika kwa lengo la kuimarisha uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mfumo wa *NeST,* kuna kategoria mbalimbali za wazabuni ambapo kampuni itatambuliwa na Mfumo wa *NeST* kama kampuni ya ndani endapo kampuni hiyo imesajiliwa Tanzania; inamilikiwa na raia wa Tanzania kwa 100% au raia wa Tanzania anamiliki mtaji wa hisa katika kampuni hiyo zisizopungua 51%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa timu ya ujenzi wa Mfumo wa *NeST* inakamilisha ujenzi ndani ya mfumo wa namna ya kutekeleza masuala ya upendeleo kwa wazawa. Hivyo, utekelezaji wa sharti la upendeleo kwa wazawa ndani ya Mfumo wa *NeST* linatarajiwa kuanza Julai, 2025. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 inazitaka taasisi za Serikali kutenga 30% ya bajeti kwa ajili ya makundi maalum; 10% kwa vijana, asilimia tano kwa wanawake, asilimia tano kwa wazee na 10% kwa watu wenye ulemavu. Je, makundi hayo yana uelewa kiasi gani wa kuzifikia hizo fursa na jinsi ya kupata hizo *tender? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa kuwa kuna wakati Serikali huwa inachelewesha malipo kwa wakandarasi na kusababisha wakandarasi hao kuuziwa dhamana zao katika benki. Je, sasa Serikali haioni umuhimu wa kuwapatia benki *guarantee* ili hawa wakandarasi wa ndani na wazabuni wasiweze kuuziwa dhamana zao katika benki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Kabati, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu maswali hayo, ninaomba nimpongeze sana kwa namna anavyofuatilia taratibu hizi za *NeST* na 30% iliyowekwa katika makundi maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imetoa 30% kwa makundi maalum wakiwemo vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Serikali tayari imetoa maelekezo kwa taasisi zote nunuzi wafuate sheria hiyo ambayo imewekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uelewa kwa makundi hayo, Serikali kupitia *PPRA* inaendelea kutoa mafunzo mbalimbali, inaendelea kutoa semina na warsha, kwa mfano, hivi karibuni katika Jiji la Arusha Serikali kupitia *PPRA* imetoa mafunzo kwa makundi hayo, lakini Mwanza pia imetoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunavyozungumza katika viunga hivi vya Bunge wapo wataalam wetu wa *PPRA* katika eneo eletu hili wanatoa maarifa hayo na uelewa. Kwa hiyo, niombe tu Waheshimiwa Wabunge na wenyewe nao wawe mabalozi wa kuelimisha watu wetu katika sehemu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili, ninaomba nimtoe shaka kabisa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwamba Serikali itaendelea kulipa kwa wakati na wale ambao wamechelewa kwa bahati mbaya tu, basi watalipwa na wataendeleza biashara yao kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wake tumepokea pia kwamba Serikali iweze kuingilia kati jambo hilo, basi Serikali itafanya hivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma Kikwete. Ninaomba uniwie radhi.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Maida.

**MWENYEKITI:** Ni Maida? Umekaa kiti cha mtu ninadhani. *(Makofi)*

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa benki za kibiashara nchini hutoa mikopo kwa riba kubwa kwa wakandarasi nchini; je, Serikali ina mkakati gani madhubuti na mpango maalumu wa kuwapatia mikopo wakandarasi kwa masharti nafuu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Maida kwa namna anavyofuatilia unafuu wa wananchi. Serikali tayari imeshatoa maelekezo kwamba wakandarasi wetu hasa wazawa wanapokwenda katika benki zetu za kibiashara wapewe mikopo kwanza stahiki lakini na kwa riba nafuu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata. Swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Husna Sekiboko.

Na. 530

**Kurasimisha Biashara za Sekta Isiyo Rasmi Nchini**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO K.n.y. MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza: -

Je, Serikali imepiga hatua gani katika kurasimisha biashara za sekta isiyo rasmi ili kuongeza uchumi wa nchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali kupitia *TRA* ina utaratibu wa kuwatambua walipakodi kulingana na mitaa *(Blocks Management System)* ambayo husimamiwa na maofisa kodi ambao hutembelea mitaa husika na kufanya ukaguzi kwa wafanyabiashara ili kujua mwenendo wao katika kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali kupitia *TRA* imeendelea kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara wadogo wadogo pamoja na kuwapa elimu juu ya huduma za kikodi ikiwa ni pamoja na *TIN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, *TRA*, TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maendeleo na Makazi na Mifuko ya Kijamii na Wizara ya Viwanda, ipo katika zoezi la ugawaji wa vitambulisho vya kijiditali kwa wafanyabiashara ndogo ndogo kwa lengo la kuwatambua, kuwawezesha kimitaji na kufuatilia kwa karibu maendeleo ya biashara zao. Lengo la mkakati huu ni kuwakuza wafanyabiashara na hatimaye kuwaingiza kwenye mfumo rasmi ambao wataweza kusajiliwa na kulipa kodi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yamejibu hoja zote ambazo nilitaka nihoji hapa. Niiombe tu Serikali, huu mpango wa kuwa na kanzidata kwa ajili ya kuwatambua wale vijana wote na baadaye kuwawezesha, basi ufanyike kwa haraka ili vijana hao waweze kunufaika na mpango huo. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sekta isiyo rasmi ambayo inabeba wajasiriamali wa aina mbalimbali inakabiliwa na changamoto kubwa ya mitaji ya kifedha. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuzishawishi benki za kibiashara zianzishe madirisha ambayo yatawasaidia hawa watu kupata mikopo ili waweze kuanzisha biashara na kukuza biashara zao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, unaweza kupokea ushauri wa Mheshimiwa Sekiboko na ukajibu swali la Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaomba nipokee ushauri wa Mheshimiwa Sekiboko. Ushauri wake umechukuliwa na utaenda kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, lakini tayari Serikali imeshatoa maelekezo kwa benki za kibiashara kuwaita watu hao na kuwafuata wajasiriamali wetu kuwapa mafunzo, lakini na kufungua madirisha madogo madogo kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya watu wetu, yaani wajasiriamali wadogowadogo. Kwa hiyo, nikutoe shaka kwamba jambo hilo Serikali imelizingatia na litaenda kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 531

**Elimu ya Vifungashio kwa Wajasiriamali Wadogo**

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu kwa wajasiriamali wadogo ili kuwawezesha kuwa na vifungashio bora vya bidhaa zao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Viwanda *(SIDO)* inatekeleza mkakati wa mafunzo ya ufungashaji wa bidhaa kwa wajasiriamali ikiwemo namna ya kutengeneza vifungashio, kutumia chapa *(brand)* na *label*. Vilevile *SIDO* inatoa elimu kwa waundaji *(designers)* na wachapaji wa *label* za bidhaa ili kuwaongezea ujuzi katika kuwahudumia wajasiriamali. Lengo la mafunzo hayo ni kuboresha vifungashio vya bidhaa za wajasiriamali ili ziweze kushindana sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *SIDO* hununua vifungashio kwa jumla *(bulk procurement)* kutoka nje ya nchi na kuviuza kwa rejareja na kwa bei nafuu katika Ofisi za *SIDO* za Mikoa kwa wajasiriamali. Hatua hiyo huwawezesha wajasiriamali kupata vifungashio bora na kwa bei nafuu, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tamima.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vifungashio duni vinashusha hadhi ya bidhaa na pia huhatarisha usalama wa chakula. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuwashajiisha wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo wadogo walioko vijijini ili kuweza kutumia vifungashio bora? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Tamima kwa ufuatiliaji na hasa kwenye sekta hii ya biashara na hasa kwa wajasiriamali amekuwa

akifuatilia sana na kuwasemea, lakini zaidi nishukuru kwa sababu anatuongezea kuhakikisha tunaboresha huduma kwa wajasiriamali na hasa kwenye vifungashio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake, ni kweli vifungashio duni au ambavyo havina ubora vinapunguza ubora na ushindani wa bidhaa zetu na hasa za wajasiriamali. Sasa ametumia Kiswahili kizuri kwamba kwa nini tusiwashajiishe wajasiriamali, ninadhani anamaanisha tuendelee kuwafahamisha au kuwafundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi kubwa tunayofanya sasa na haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha bidhaa zetu au wajasiriamali au sekta binafsi ya ndani inakuwa shindani. Kwa hiyo, kupitia *SIDO* tunafanya kazi hiyo, kuwasaidia; kwanza, kuwafundisha lakini pili, kuwasaidia kutengeneza kama nilivyosema vifungashio hivyo vikiwa na ubora lakini pia kuweka *label* kwa sababu wengine walikuwa wanatengeneza vifungashio vile bila kuonesha kwamba imetengenezwa na nani na wapi, lakini pia kuwa na rangi kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaendelea kuusimamia ubora wa vifungashio ili kweli bidhaa zao ziweze kuwa na ubora, kwa sababu unavyofungasha bidhaa ndiyo itaonesha ubora wa bidhaa iliyo ndani kutokana na kifungashio ambacho umekitumia, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni kweli *SIDO* wanatengeneza vifungashio vilivyo bora, lakini nini mkakati wa Serikali kuunganisha juhudi zake pamoja na Shirika la Viwango, kwa sababu vifungashio vinaweza kuwa bora, lakini zile *contents* zinapimwaje, kwa sababu nyingi ni za vyakula. Sasa Serikali mnafanya nini kuunganisha juhudi zenu na *TBS* kuwafahamisha kwamba hawa watu wana umuhimu pia

hivyo wanavyovitia ndani vikapate ubora na kuhakikishwa na *TBS*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Asha Abdullah Juma kwa swali hili zuri, lakini na yeye amekuwa mdau mkubwa sana hasa kwenye sekta ya ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali tuna mkakati maalum na hasa hili tunalisema kwa sababu bahati nzuri taasisi alizozitaja zote ziko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, *SIDO* na *TBS* kuna mkakati maalum ambao unatumika, kwanza kwa kuwatengea fedha wajasiriamali wadogo zaidi ya milioni 350 katika bajeti ya mwaka tunaweka kwa ajili ya wajasiriamali. Na mambo mengine ambayo yanaangaliwa ni ubora wa bidhaa ikiwemo na hizi za vifungashio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inafanya kazi kubwa kuhakikisha ubora wa bidhaa lakini pia na vifungashio unasimamiwa na *TBS* kwa kushirikiana na *SIDO* ili kuhakikisha yale mafunzo na bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali zinakidhi ubora na zinakuwa shindani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu Mbunge wa Geita Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Tumaini Magessa.

Na. 532

**Uwepo wa Ajali Nyingi katika Mji wa Geita**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA K.n.y. MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza: -

Je, upi mpango wa Serikali kuokoa maisha ya wananchi kutokana na uwepo wa ajali nyingi katikati ya Mji wa Geita maeneo ya Nyankumbu na Shilabela?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mkoa wa Geita kwa kushirikiana na *TANROADS* pamoja na Jeshi la Polisi wamekubaliana kuendelea kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya barabara kwa wananchi na madereva wa vyombo vya moto. Katika eneo la Nyankumbu yamewekwa matuta pamoja na alama ya mwendokasi wa kilometa 50 kwa saa ili kupunguza ajali na kuokoa maisha ya wananchi kwa kuwa eneo hili pamoja na eneo la Shilabela ni maeneo yenye watu wengi na shughuli nyingi za kiuchumi. Aidha, Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inaendelea na utoaji wa elimu kwa umma juu ya kinga na tahadhari dhidi ya majanga mbalimbali katika mji wa Geita. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tumaini Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kuhusu elimu inayoendelea kutolewa kwenye maeneo haya ambayo watu wengi wanapoteza maisha nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, je, Serikali imefanya utafiti wa kutosha kujua kwamba ajali hizi zinazotokea inawezekana zikawa zinasababishwa na tatizo la kihandisi *(engineering problem)*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa vile pale Nyankumbu kuna soko na vilevile kuna shule, kwa hiyo, wanafunzi wengi wanaopita maeneo hayo na hao wanaoenda sokoni wanagongwa mara kwa mara.

Je, nini mpango wa Serikali kuanza kuweka mazingira ambayo yanaweza kujengwa daraja la juu *(fly over)* ili kuondoa kabisa tatizo hili la wananchi kugongwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Magessa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza suala la usalama barabarani ni suala la wadau wengi; kwanza watumiaji wa barabara, watembea kwa miguu, lakini madereva wa vyombo vya moto, pamoja na Jeshi la Polisi kwa maana ya Kikosi cha Usalama Barabarani. Kwa hiyo, nitoe kwanza wito kwa wale wadau wote hawa kama nilivyojibu jibu la msingi kuzingatia Sheria za Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu pengine ni tatizo la kiufundi; sote ni mashahidi kwamba barabara zinavyojengwa kwanza unafanyika usanifu wa kina kuhakikisha kwamba inajengwa kwenye viwango, lakini kwa kuwa ajali hiyo imeendelea kutokea, pamoja na kutoa elimu kwa umma lakini pia Serikali itaendelea kufanya utafiti na kuona kama changamoto hiyo inatokana na suala la kiufundi. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba ama tunapunguza au kumaliza kabisa ajali za usalama barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, ujenzi wa daraja la juu; Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi itafanya utafiti na tathmini kuona kama kuna haja ya kujenga daraja la juu. Lengo letu la msingi kama nilivyosema ni kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaepuka ajali ambazo siyo za lazima ili kuokoa usalama wao waendelee kuwa salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wengi hawana elimu ya kutosha ya namna ya kukabiliana na majanga yoyote yale yanapotokea na hata ikitokea hawajui nini wafanye, kwa sababu hawana hiyo elimu, lakini hata wanafunzi wetu kuanzia shule za msingi mpaka sekondari hawapati hiyo elimu vya kutosha.

Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba, elimu inatolewa ili kuwaokoa wananchi wetu pale ambapo majanga yanatokea au kuzuia wasikutane na majanga mbalimbali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa elimu hasa kwenye shule za msingi na sekondari juu ya kuchukua tahadhali mbalimbali hasa kwenye masuala ya zimamoto na uokoaji. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kutoa elimu hiyo kuhakikisha kwamba hasa kwenye shule za msingi kule chini kabisa na shule za sekondari ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wanapokua wanakuwa wanaelewa sana kujikinga na ajali mbalimbali au majanga yanavyotokea katika maeneo yetu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana, ninakushukuru sana.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, nimesimama kwa Kanuni ya 76, jambo lililotokea leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ninaomba nisome kwa ufupi ili tuweze kuelewa. Kanuni ya 76 inasema, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo lililotokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema leo asubuhi niliuliza swali la nyongeza kwenye Wizara ya Ardhi, nikieleza mgogoro wa ardhi unaotokea Kilimanjaro na hata wakati ninaongea sasa kuna mgogoro wa ardhi unaendelea Wilaya ya Hai, Moshi Vijijini kwenye Shamba la Laitoria, unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza kama Mbunge kwa mujibu wa Katiba na ninaelewa Bunge letu linafuata Katiba, ndani ya Bunge kuna Wabunge wa Viti Maalum, kuna Wabunge wa Majimbo, kuna Wabunge wa Kuteuliwa na Rais, kuna Wabunge ambao ni Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi, lakini kuna Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba, Bunge letu, Wabunge hawa hawajapewa wigo kwamba mwisho wako wa kuuliza swali ni hapa. Tumepewa utaratibu wa kuishauri Serikali na kuweza kuisimamia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista Njau, jielekeze kwenye hoja yako tafadhali.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa ninaelekea kwenye Mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninauliza swali, Mheshimiwa Naibu Waziri hakuni-*address* swali langu kabisa, maana yake

hakunijibu mimi. Alikuwa anaongea anamtaja Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo, ninafurahi akimu-*address*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba anijibu mimi, kwa sababu sikutendewa haki, hakunijibu swali langu alimu-*address* Mbunge wa Jimbo, akazungumza mwanzo-mwisho, wala hakunijibu. Nami nimetumwa na wananchi kwa mujibu wa Katiba, nina haki ya kupewa nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wako kama nimetendewa haki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasimama kwa Kanuni ya 76 na sitoitaja, lakini pia ninajielekeza katika Kanuni ya 53(1). Kanuni ya 53 ambayo inaeleza kujibiwa swali kikamilifu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nimeuliza swali leo namba 528, na swali langu lilikuwa limeuliza kwamba, Serikali imepoteza mapato kiasi gani tangu mwaka 2015 mpaka mwaka 2020. Lakini, kwanza nipongeze kwamba wameeleza kuna ongezeko la 400% kwenye makusanyo ya Serikali baada ya mifumo ya TEHAMA kufungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka nifahamu pamoja na ongezeko hilo la shilingi trilioni 2.21, ninataka nifahamu katika hiyo tangu tumefunga mifumo amesema tumeongeza kiasi gani, je tumepunguza kiasi gani, tumeokoa kiasi gani. Ili tuone sasa kama tunaweza kushauri Serikali wapi iongeze nguvu. Sasa swali langu halijaenda kwenye kipengele cha pili, limeishia kwamba tumeongeza mapato kwa 400%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba Mwongozo wako kwa sababu swali langu halijajibiwa kikamilifu, siyo kitu nilichoomba katika swali ili sasa ukituelekeza kama watarudi walijibu labda halikueleweka na wamefanya jitihada na ndiyo maana nimepongeza, lakini ninatamani tufahamu kwa mujibu wa

ripoti ya *CAG* pia alieleza kwamba, kuna upotevu katika makusanyo kwenye mifumo ya TEHAMA na Mheshimiwa Rais alielekeza wakaongeze nguvu katika utatuzi. Sasa ninataka kufahamu Serikali imepoteza kiasi gani tangu mwaka 2015 mpaka 2020. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwanza alisimama Mheshimiwa Felista Njau, Mbunge wa Viti Maalum kwa kanuni ya 76 akieleza kwamba hajatendewa haki wakati Mheshimiwa Waziri akijibu swali la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, alitaka kujua kama hili jambo linaruhusiwa au haliruhusiwi. Sasa kwa sababu swali hili halikuwa swali la msingi na kwa vile swali la nyongeza huwa halina majibu ya maandishi mezani, majibu ya maandishi yanaletwa kwa jibu la msingi, swali la nyongeza halina majibu mezani. Kwa hiyo, ili kuweza kuthibitisha kama jambo hili linaruhusiwa au haliruhusiwi ni lazima turejee kwenye *Hansard* za Bunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo Mheshimiwa Felista Njau, kiti kitafanya rejea kwenye *Hansard* na kwa utaratibu wa Kibunge utapata majibu kama yale yaliyojibiwa yanaruhusiwa au hayaruhusiwi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia alisimama Mheshimiwa Nusrat Hanje kwa kanuni hiyo hiyo ya 76 akieleza kwamba majibu yaliyotolewa kwa swali namba 528 hayatoshelezi na hajajibiwa kikamilifu. Tofauti na maswali ya nyongeza, maswali ya msingi huwa yanajibiwa kwa maandishi na hapa ninayo maandishi ya majibu ya swali lake.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mbunge alitaka Serikali imueleze kuhusu kupotea kwa fedha. Swali lake linasema; je, Serikali imepoteza fedha kiasi gani tangu mwaka 2015 - 2020 kwa kutokuwepo usalama madhubuti wa mifumo ya usimamizi kufuatia mabadiliko ya TEHAMA duniani?

Waheshimiwa Wabunge, majibu ya Mheshimiwa Waziri yanaeleza, sitayasoma yote ila yanaeleza kwamba Wizara, Idara

na Taasisi mapato yameongezeka kutoka shilingi bilioni 689 mwaka 2014/2015 shilingi trilioni 2.21 mwaka 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la 400%.

Waheshimiwa Wabunge, *it goes without saying* na *logic* inatuambia kwamba mapato hayajapungua, mapato yameongezeka, kwa hiyo, hakuna upotevu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo Mwongozo wa Kiti kwa sasa. Na baada ya hapo ninaomba mniruhusu nitangaze wageni ambao tunao Bungeni.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni 58 wa Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Mbunge na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni Wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri ya Wilaya ya Butiama, Watendaji wa Kata za Halmashauri ya Wilaya ya Butiama na wafanyabiashara kutoka Wilaya ya Butiama Mkoani Mara. Kama wapo tunaomba wasimame, karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Balozi Liberata Rutageruka Mulamula, Mbunge ambao ni Kamati ya Utekelezaji UWT Wilaya ya Missenyi Mkoani Kagera, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ambao ni Waandishi wa Habari *Vibes FM* kutoka Katoro, Mkoani Geita. Kama wapo karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 42 wa Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Mbunge ambao ni Kwaya ya Uinjilisti Usharika wa Bethel kutoka Kanisa la KKKT Sae, Mkoani Mbeya, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 36 wa Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge ambao ni walimu wa Shule ya Awali na Msingi *Lightness* kutoka Wilaya ya Manyoni, Mkoani Singida. Kama wapo karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 36 wa Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Kama wapo karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 14 wa Mheshimiwa Mhandisi Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge ambao ni wapigakura wake kutoka Hanang Mkoani Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 110 wa Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge, ambao ni walimu wa Shule ya Msingi Aldesgate kutoka Babati, Mkoani Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; ambao ni wanachama 31 wa Kikundi cha Kijamii cha *Bring and Share Group* kutoka Kibaha, Mkoani Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Shughuli za Bunge zitaendelea kwenye kumbi zetu maalum za kazi zinazohusu mijadala kati ya Serikali na Kamati za Bunge.

Kwa hiyo, ninaahirisha Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 4.56 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya* Jumatatu, *Tarehe 9 Juni, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*